

Kutunza meno na fizi za mtoto wako

Umri wa chini ya miezi 18

Ikiwa mtoto wako hapendi kupiga mswaki, unaweza kujaribu kufanya shughuli ya kupiga mswaki iwe ya kufurahisha zaidi kwa kuimba nyimbo au kumruhusu mtoto wako achezze na mdoli. Hata jaribio la haraka la kupiga mswaki ni bora kuliko kutofanya chochote, hivyo mtoto wako anaanza kujifunza kwamba kupiga mswaki ni sehemu ya kawaida ya utaratibu wake wa kila siku.


Kuanza utaratibu mapema humpa mtoto wako nafasi nzuri ya kuwa na meno yenye afya.

Nitaanza lini kutunza meno ya mtoto wangu?



Mara tu jino la kwanza la mtoto wako linapoonekana, piga mswaki kwa upole kwa kutumia mswaki mdogo na laini. Au unaweza kupangusa kwa kiocha-uso chenye unyevu na safi badala yake.

Piga mswaki au upanguse meno kwa maji hadi mtoto wako afikishe umri wa miezi 18.



Hata kabla ya meno kuonekana, unaweza kupangusa fizi za mtoto kwa kutumia kiocha-uso chenye unyevu na safi. Hii inaweza kusaidia kuandaa mtoto wako kwa ajili ya kupiga mswaki.

Je, nitaanza lini kutumia dawa ya meno?



Mtoto wako anapokuwa na umri wa miezi 18 piga mswaki kwa dawa ya meno ya watoto yenye floridi kidogo.

Je, mimi napaswa kupiga mswaki meno ya mtoto wangu mara ngapi?




Piga mswaki asubuhi na usiku kabla ya kulala.





Piga mswaki asubuhi na usiku kabla ya kulala.
Tumia kiasi cha njegere cha dawa ya meno ya watoto yenye floridi kidogo kwenye mswaki laini.



Sugua sehemu za nje kwa mtindo wa miduara taratibu.



Kisha, sugua sehemu za ndani kwa mtindo wa miduara taratibu.



Tumia mwendo mwepesi wa kwenda na kurudi kwenye sehemu za kutafuna, juu na chini.



Mwambie mtoto wako ateme dawa ya meno wala asisuuze kwa maji.

Kutosuuza dawa ya meno yenye floridi husaidia kulinda meno.

Jinsi ya kupiga mswaki meno ya mtoto wako

Miezi 18 hadi miaka 6

Vidokezo:

- Chagua mkao unapoweza kuona meno ya mtoto wako Jaribu mikao tofauti inayofaa kwako na mtoto wako.
- Kadiri mtoto wako anavyojitegemea zaidi acha apige mswaki mwenyewe. Malizia kwa kupiga mswaki mwenyewe.
- Watoto wanahitaji kusaidiwa kupiga mswaki hadi angalau umri wa miaka 8.

